Athletics Integrity Unit

# U20

# MWONGOZO WA UADHILIFU



Mwongozo huu wa uadilifu unajumuisha taarifa muhimu za uadilifu katika michezo kwa wanariadha na wasaidizi wa wanariadha.

Masuala ya uadilifu yanaweza kuathiri taaluma yako, timu yako na maisha yako ya baadaye. Iwapo unahisi jambo si sahihi, usilipuuze.

## AIU ni nani?

Kitengo cha Uadilifu wa Riadha (AIU) ni chombo huru kilichoanzishwa na World Athletics kusimamia masuala yote ya uadilifu— matumizi ya dawa za kusisimua misuli na yasiyohusiana na dawa hizo—katika mchezo wa riadha.

# Tuna..

shirikisha
saidia
wezesha

tetea
elimisha
wasilisha taarifa

pima
chunguza
fungua mashtaka

## AIU inasimamia masuala mbalimbali ya maadili, yakiwemo:

- Kupambana na matumizi ya dawa za kusisimua misuli
- Udanganyifu wa umri
- Udanganyifu / uchepusaji  matokeo ya mashindano
- Ukiukaji wa kanuni za kubashiri
- Udanganyifu unaohusiana na kubadilisha nchi ya uwakilishi
- Unyanyasaji na ukatili
- Hongo na ufisadi

# Matumizi ya dawa za kusisimua misuli ni nini?

Matumizi ya dawa za kusisimua misuli si tu kuwa na kipimo chenye matokeo chanya. Hufafanuliwa kama kutokea kwa ukiukaji mmoja au zaidi wa kanuni za kupambana na dawa za kusisimua misuli (ADRV). Ukiukaji wote 11 ufuatao unawahusu wanariadha; ukiukaji 7 unawahusu wasaidizi wa wanariadha (ASP) au watu wengine.

1. Kuwepo kwa dawa iliyopigwa marufuku, metaboli zake au viashiria vyake katika sampuli ya mwanariadha.
2. Matumizi au jaribio la kutumia dawa au mbinu iliyopigwa marufuku na mwanariadha.
3. Kukataa, kukwepa au kushindwa kutoa sampuli kwa ajili ya uchunguzi.
4. Kushindwa kuwasilisha taarifa za mahali alipo mwanariadha na/au kukosa vipimo.
5. Kuharibu au kujaribu kuharibu mchakato wa udhibiti wa matumizi ya dawa za kusisimua misuli.
6. Kumiliki dawa au mbinu iliyopigwa marufuku kwa mwanariadha au wasaidizi wao.
7. Kusambaza au kujaribu kusambaza dawa au mbinu iliyopigwa marufuku.
8. Kumpa au kujaribu kumpa mwanariadha dutu au mbinu iliyopigwa marufuku.
9. Kushiriki au kujaribu kushiriki katika ukiukaji wa ADRV.
10. Ushirika uliopigwa marufuku kati ya mwanariadha au mtu mwingine na ASP aliyewekewa adhabu.
11. Vitendo vya kukatisha tamaa au kulipiza kisasi.

# Orodha za dawa na mbinu zilizopigwa marufuku.

Orodha ya wakala wa dunia wa kupambana na dawa za kusisimua misuli (WADA) inaeleza na kufafanua dutu na mbinu zilizopigwa marufuku wakati wa mashindano na wakati wote. Husasishwa angalau kila mwaka na huanza kutumika tarehe 1 Januari kila mwaka.

Wanariadha wana wajibu wa kujua dawa na mbinu zilizopigwa marufuku. Pia wanawajibika binafsi kwa dawa yoyote iliyopigwa marufuku inayopatikana mwilini mwao, bila kujali nia yao.

→ Angalia orodha hapa

# Ni wajibu wako binafsi

## Kuchukua tahadhari unapotumia dawa:

1. Mjulishe daktari wako kwamba unatakiwa kufuata Kanuni za WADA.
2. Hakikisha dawa zako hazina dutu zilizopigwa marufuku.
   → Global DRO
3. Thibitisha iwapo Ruhusa ya Matumizi ya Tiba (TUE) inakuhusu; ikiwa inakuhusu, tuma ombi mapema iwezekanavyo.

## Kuwa mwangalifu sana unapotumia virutubisho:

1. Chagua virutubisho kutoka kwa muuzaji anayeaminika.
2. Hakikisha virutubisho vimeidhinishwa na vimepimwa.
   → Informed Sport, Hasta, NSF

- Hifadhi kumbukumbu ya dawa na virutubisho vyote unavyotumia.
- Taja kwa uwazi kwenye Fomu ya Udhibiti wa Dawa za Kusisimua Misuli.

# Udanganyifu wa umri ni nini?

Udanganyifu wa umri hutokea mwanariadha anapobadilisha umri wake kwa namna yoyote ili aonekane mkubwa au mdogo zaidi, kwa lengo la kupata faida ya kimashindano au kifedha.

Wanariadha, maafisa na wasaidizi wa wanariadha wanapaswa kujilinda dhidi ya udanganyifu wa umri, kwa hivyo  mwenendo wako ni muhimu sana.

# Unaweza kufanya nini kuzuia udanganyifu wa umri?

- Kuwa mkweli kuhusu umri wako na tarehe yako ya kuzaliwa. Usijaribu kupata nyaraka za kughushi wala kuruhusu wengine wazipate kwa niaba yako.

- Shirikisho na ASP wanapaswa kuhakikisha kuwa tarehe ya kuzaliwa au umri umeandikwa kwa usahihi wanapomsajili mwanariadha katika mashindano au hifadhidata rasmi.

- Shirikisho na ASP wanapaswa kufanya ukaguzi wa kina na wa mara kwa mara wa nyaraka za utambulisho za wanariadha waliosajiliwa, na kuhakikisha taarifa zake zinaendana na data iliyopo.

Ikiwa mtu yeyote atakuomba ubadilishe tarehe yako ya kuzaliwa au umri wako, kataa kushiriki na uripoti kwa AIU. 🚨

# Udanganyifu wa mashindano ni nini?

Udanganyifu wa mashindano ni jaribio lolote la kudhibiti matokeo ya mashindano au kubadilisha mwenendo wa kawaida wa tukio la michezo, au sehemu yake. Unaweza kufanywa kwa faida ya kimichezo au kifedha, na wakati mwingine kupitia shughuli haramu za kubashiri au kamari.

Unaweza kujumuisha kubadilisha matokeo, kupanga michezo, ufisadi, kutocheza kwa kiwango kinachotarajiwa, au kushiriki taarifa za ndani na watu wasioidhinishwa.

# Kanuni kwa wanariadha, maafisa na wasaidizi wa wanariadha

- Ripoti njia yoyote ya kushawishi au kupanga udanganyifu wa mashindano mara tu unapoigundua

- Shirikiana kikamilifu na uchunguzi wowote unaofanywa.

- USIBASHIRI kwenye mashindano ya riadha.

- USISHIRIKI taarifa za ndani—yaani taarifa unazojua wewe au watu wachache katika riadha, lakini ambazo umma kwa ujumla hauzijui.

- USIKUBALI jambo lolote linalojaribu kubadilisha matokeo ya mashindano au linalokupa wewe au mtu mwingine faida isiyo ya haki.

- USITOE, USITAFUTE wala USIPOKEE manufaa yanayohusiana na udanganyifu wa mashindano au aina nyingine yoyote ya ufisadi

# Udanganyifu unaohusiana na kubadilisha nchi ya uwakilishi

Mwanariadha anapobadilisha rasmi nchi anayowakilisha katika mashindano ya kimataifa, mchakato huo lazima ufuate utaratibu madhubuti unaodhibitiwa na World Athletics.

Kuna hatari kadhaa za uadilifu zinazohusiana na mchakato huu ambazo zinaweza kusababisha udanganyifu unaohusiana na kubadilisha nchi ya uwakilishi: kughushi nyaraka, kuwakilisha nchi kabla ya wakati unaoruhusiwa, uwezekano wa usafirishaji haramu wa watu, kulazimishwa kutumia dawa za kusisimua misuli, ahadi za uongo au zisizotekelezwa, na kuathiriwa kwa haki na ustawi wa jumla wa mwanariadha baada ya uhamisho.

Jihadhari na hatari hizi. Kabla ya kufanya uamuzi wowote, zungumza na shirikisho lako la kitaifa na uhakikishe unaelewa kanuni zote kikamilifu.

# Michezo salama

Kanuni za World Athletics za Ulinzi na Usalama hutoa mfumo kwa wanariadha na  wasaidizi wao ili kuhakikisha mazingira salama na yenye msaada kwa washiriki wote wa mchezo wa riadha.

Kuunda mazingira salama na ya kukaribisha, ambako kila mtu anaheshimiwa na kuthaminiwa, ni kiini cha ulinzi na usalama.

Kila anayeshiriki katika riadha ana wajibu wa kusaidia kuzuia ukatili, unyanyasaji au unyonyaji dhidi ya washiriki katika mchezo

Jua haki na wajibu wako ili ujilinde na kulinda  wengine.

AIU
Integrity
Line

# Timiza wajibu wako kwa kuripoti ukiukaji wowote wa kanuni

Shiriki taarifa kwa usalama na AIU wakati wowote. Unaweza kufanya hivyo kisiri bila kutaja jina lako; hatutaona maelezo yako ya mawasiliano isipokuwa uchague kuyafichua.

## WhatsApp

Ongea na sisi kwa kisiri.
hatuwezi kutambua nambari,jina au picha lako.

## Barua Pepe

Unaweza kubaki bila kutambulika ukipenda

## Fomu ya Mtandaoni

Wasilisha fomu salama ya mtandaoni.
Kumbuka ufuonguo wako wa arifa. ili uweze kupokea majibu yetu.

Huhitaji mtizamo wa “kushinda kwa gharama yoyote” ili kuwa na mtizamo wa bingwa.

Katie Moon

Bingwa wa Dunia,  Bingwa wa Olympiki



# Tuandikie

## Tuko hapa kukusaidia!

Iwapo una wasiwasi au maswali yoyote, usisite kuwasiliana na Kitengo cha Uadilifu wa Riadha (AIU).

education@athleticsintegrity.org

athleticsintegrity.org

aiu_athletics